UNITED
EVANGELICAL
MISSION

kiswahili

# Codes of Conduct

(CoC)

For the full Codes of Conduct please visit:

**www.vemission.org/en/downloads/uem-rules**

# Dear readers,

it is important to us that whenever you come into contact with the UEM, whether as an employee, visitor, participant, donor or recipient, you can rely on a non-discriminatory, safe and transparent environment.

Our three Codes of Conducts (CoC) provide us with guidelines and instructions on how to behave in order to achieve precisely this goal.

These are

**CoC against sexualised harassment and violence**
**CoC against racism and discrimination**
**CoC for transparency and against corruption**

To make it easier to access these documents, we have summarised these Codes of Conducts and translated them into the easiest possible language to facilitate access to this important information. The document you are holding in your hands is available in English, German, Swahili, Indonesian and French – feel free to ask us about it.

We hope these Codes of Conducts are clear and helpful to you

***The Management Team of UEM***

November 2025

You can find the CoCs in full length online here:

# Kanuni za Maadili Dhidi ya Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia

**Biblia inathibitisha hadhi ya asili na thamani ya kila mtu, ikisisitiza upendo, heshima, na kuheshimiana katika mahusiano. Katika muktadha wa unyanyasaji wa kijinsia, Biblia inakemea kila aina ya unyanyasaji au udhalilishaji wa watu wengine. Waefeso 5:3 inahimiza usafi na heshima pande zote, ikionyesha kwamba matendo yanayomdhalilisha au kumuumiza mtu mwingine ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Biblia inatuhimiza kuwatendea wengine kama tunavyotaka watutendee, ikikuza haki na ulinzi kwa walio hatarini.**
**UEM na wanachama wake wanakubaliana kwamba unyanyasaji wa kijinsia ni ukiukaji mkubwa wa haki na hauna nafasi katika jamii ya UEM.**
**Lengo la Kanuni hizi za Maadili ni kuthibitisha upya dhamira ya UEM ya kuunda mazingira salama na yenye heshima kwa wafanyakazi wote wa UEM na washiriki wa shughuli zake. Wafanyakazi na wasimamizi wote wana wajibu wa kushughulikia na kuzuia unyanyasaji wa kijinsia.**

## Jinsi ya Kuepuka Unyanyasaji wa Kijinsia

1. Heshimu mipaka inayowekwa na wengine. “Hapana” ni jibu kamili na linapaswa kuheshimiwa bila maelezo zaidi.
2. Kuwa makini na tofauti kati ya watu. Kile kinachoweza kukubalika kwa mtu mmoja chaweza kuwa kero au kisichofaa kwa mwingine. Hakikisha matendo na maneno yako ni yenye heshima na yanazingatia ustawi wa kila mtu.

### Ufafanuzi

Kimsingi, kuna aina tatu za unyanyasaji wa kijinsia:

1. **Unyanyasaji wa maneno:** Kauli za kejeli, maoni yenye maana fiche, maswali yasiyofaa kuhusu maisha binafsi au mambo ya faragha, mwaliko wa kimapenzi usiotakiwa, au maombi ya vitendo vya kimwili vya ngono.

2. **Unyanyasaji wa ishara, bila kutumia maneno:** Kutazama kwa muda mrefu, kupiga mluzi, ishara za kudhalilisha, kutuma ujumbe, picha au video za kimapenzi zisizotakiwa, au hatua zisizofaa kwenye mitandao ya kijamii.
3. **Unyanyasaji wa kimwili:** Kugusa bila ridhaa (kama kupapasa, kupiga mabega, au kushika), majaribio ya kumbusu au kumkumbatia mtu kwa nguvu, vitendo vya uchi hadharani, au shambulio la kingono.

Unyanyasaji wa kijinsia mara nyingi hauhusiani na hamu ya dhati ya kimapenzi bali ni njia ya kutumia mamlaka na kulazimisha, ndiyo maana neno "unyanyasaji wa kijinsia" hutumika zaidi siku hizi.

## Wigo wa Matumizi

1. Kanuni hizi zinatumika katika mazingira yote ya UEM na shughuli zake zote, ikijumuisha wafanyakazi, watu wanaowakilisha UEM, na washiriki wote wa shughuli zinazofanywa na au kwa niaba ya UEM. Kanuni hizi huwasilishwa na kuelezwa mwanzoni mwa kila shughuli. Hivi dhamira ya UEM dhidi ya aina zote za unyanyasaji wa kijinsia inasisitizwa.
2. Katika mikutano rasmi ya UEM, watu wawili wa mawasiliano (mwanamke na mwanaume) huteuliwa na kutangazwa. Watapewa maelekezo na mwanachama wa Baraza au Timu ya Usimamizi, na lazima wasaini kanuni hizi.

## Majukumu ya Watu wa Mawasiliano

Kufuatilia na kuripoti:

- Fuata kwa makini shughuli zote na kuripoti mara moja visa vyovyote vya unyanyasaji wa kijinsia kwa Halmashauri.
- Hakikisha kuna nyaraka kamili za visa vyote, huku ukiheshimu faragha ya waliohusika.

Kutoa mazingira salama:

- Toa nafasi salama na ya msaada kwa watu kuripoti unyanyasaji.
- Sikiliza kwa makini bila kuhoji au kuhukumu.

- Wahakikishie wanaotoa taarifa kuwa madai yao yanachukuliwa kwa uzito na ustawi wao ni kipaumbele.

Kudumisha usiri:
- Shughulikia taarifa zote kwa usiri mkali. Usifichue habari bila ridhaa ya mtu aliyeathiriwa.
- Linda hadhi na faragha ya mtu huyo wakati wote.

Kujadili hatua zaidi:
- Jadili kwa pamoja na mtu aliyeathirika kuhusu hatua zinazofuata.
- Toa mapendekezo lakini chukua hatua tu kwa ridhaa yake.
- Heshimu maamuzi yake katika mchakato mzima.

Ufuatiliaji na msaada:
- Toa msaada endelevu, ukihakikisha mtu ana rasilimali na msaada anaohitaji.
- Fuatilia mara kwa mara hali yake na maendeleo ya kesi iwapo ipo.

## Mwongozo wa hatua zaidi

UEM inahimiza kuripoti matukio ya unyanyasaji mara moja bila kuchelewa. Hakutakuwa na adhabu kwa wanaoripoti.

1. Mtu aliyeathiriwa anapaswa kwanza kumhusisha mtu anayemwamini, ambaye anaweza kuwa mtu wa mawasiliano au mtu mwingine yeyote.
2. Kwa pamoja, wanaweza kuamua hatua zaidi, kama vile:
   a. Kuripoti kwa msimamizi, idara ya rasilimali watu, mwakilishi wa wafanyakazi, au mwanachama wa timu ya usimamizi.
   b. Kuripoti kwa chombo cha nje ya UEM.

- Wasimamizi wote wana wajibu wa kuripoti makosa yoyote kwa Sekretarieti Kuu, au moja kwa moja kwa Halmashauri ikiwa kuna shaka juu ya uadilifu. Ripoti zote zinapaswa kushughulikiwa kwa umakini na usiri.
- Iwapo mtu aliyeathiriwa ataamua kuhusisha chombo cha nje, Timu ya Usimamizi italazimika kushirikiana nacho. Hatua za kinidhamu kazini zinaweza kuchukuliwa bila vizuizi.

## Shughuli enedelevu

UEM inatoa mafunzo na mikutano ya taarifa kuhusu kuzuia unyanyasaji wa kijinsia, kuongeza uelewa, na utaratibu wa kutoa taarifa. Mafunzo haya ni lazima kwa wafanyakazi wote wa UEM.
Wafanyakazi wanahimizwa kushiriki ili kuboresha utamaduni wa kazi kwa kuendelea.

# Kanuni Dhidi ya Ubaguzi na Ubaguzi wa Mbari

**Jumuiya ya UEM imejikita katika msingi wa Kikiristo wa kuheshimiana na kuthaminiana, ambao hujifunua katika maisha yote ya binadamu ambaye ameumbwa kwa mfano wa Mwenyezi Mungu. Huu ndio msingi wa utambulisho wa Jumuiya ya UEM na jitihada zake za kupambana dhidi ya udhalimu, ubaguzi na ubaguzi wa mbari. Hivyo, Jumuiya ya UEM imejikita katika kutekeleza hatua za kimfumo za kutambua na kupambana kwa vitendo dhidi ya kila aina ya upendeleo, mazoea au fikira za kibaguzi na ubaguzi wa mbari, fikira na vitendo ambavyo ni kinyume cha imani yetu kwamba binadamu wote ni sawa mbele ya Mwenyezi Mungu, iliyojengwa juu ya msimamo wa Wanachama wote wa Umoja wa Makanisa ya Jumuiya ya UEM ili kupambania haki na amani.**

## Fafanuzi

### Upo ubaguzi wa aina mbili:

- **Ubaguzi wa Moja kwa Moja**
  Wakati mtu anapotendewa kwa upungufu wa stahiki yake kuliko mwingine anavyotendewa, alivyotendewa au ambavyo angetendewa katika hali kama ilivyo.
- **Ubaguzi fiche**
  Wakati ambapo watu fulani hubaguliwa katika mazingira ambayo yanaonekana hayana ubaguzi au hayana madhara katika muktadha wake.

### Mifano husika ni kama:

### Ukatili (kama vile unyemeleaji na uonevu)

Iwapo tabia yoyote inakusudia au inaleta athari ya kuvunja heshima ya mhusika na ikaunda mazingira ya hofu, ya kudhalilisha heshima, kumnyanyasa au yenye kuchukiza.

- Unyemeleaji una maana ya kitendo cha makusudi na kinachorudiwa au cha kikatili dhidi ya mtindo wa maisha ya mhusika na kuufanya uwe hasi au kutishia usalama wake.
- Uonevu ni ukatili wa kimfumo unaorudiwarudiwa, ukatili na utengwaji wa mhusika wenye lengo au matokeo ya kusababisha mtu huyo asiwe salama, aliyeshushiwa hadhi na kutolewa nje ya mazingira ya kazi.

### Ubaguzi wa Kimbari

Usemi "Ubaguzi wa Kimbari" una maana ya aina yoyote ya utofautishaji, utengaji, uwekaji mipaka au upendeleo unaotokana na ukabila, rangi ya ngozi, "mbari", asili au utaifa ambavyo huathiri haki za msingi za binadamu, uhuru wa msingi kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni au eneo lolote jingine la maisha ya kawaida.

### Ubaguzi wa Kingono

Hii inaweza kujitokeza katika namna nyingi: katika maneno, bila maneno au kwa vitendo halisi shambulizi kama vile lugha au ishara zinazodhalilisha mtu kingono, kwa kuonesha vitendo vichafu vya kingono, visivyofaa au maonesho ya sehemu za uchi (kama vile graffiti) kwa kutumia vitendo vya kingono visivyofaa au matakwa, na hasa, katika migusano halisi ya kingono.
Hii inaweza pia kutokana na tabia ya woga ya mtu dhidi ya maelekezo ya kimazingira au msimamo wake kuhusu ngono.
Hivyo ufafanuzi wa ubaguzi wa unyanyasaji wa kingono haukubaliki au kueleweka kwa namna ileile mahali pote- bali hutegemea hasa kutokana na watu wanaopatwa na tukio hilo.

## Maeneo ya kutumika

Kanuni hizi za Maadili zinatumika katika mazingira na shughuli zote za Jamii ya UEM. Hii inahusisha waajiriwa, watu wanaowakilisha Jumuiya ya UEM na shughuli zingine zozote zinazofanyika kwa niaba ya Jumuiya ya UEM.

## Mapendekezo ya jinsi ya utumiaji;

### 1. Vituo vya mawasiliano:

Watu waliobaguliwa au kufanyiwa ukatili au waliotendewa vurugu, wanahimizwa kuwasiliana na mojawapo ya vituo vifuatavyo ndani ya Jumuiya ya UEM:
*Wasimamizi, Watumishi wa UEM wenye mamlaka ya kushughulikia utumishi, uwakilishi wa waajiriwa, wachunguzi wa malalamiko na Wajumbe wa Baraza Kuu la Jumuiya ya UEM.* Zaidi ya hayo watu waliothirika wanaweza kuwasiliana na watu wa nje ambao wanaweza kutoa msaada wa kitaalamu katika muktadha wao mahususi.
Mwathiriwa anaweza kuamua hatua ipi ichukuliwe kwa mujibu wa Kanuni za Maadili.
Ili hatua za mchakato ziweze kuanza, malalamiko yanatakiwa yawe katika maandishi. Iwapo malalamiko yanatolewa kwa mdomo tu, inabidi yabadilishwe na kuwekwa tena katika hali ya maandishi.

### 2. Taratibu za malalamiko

Ili mchakato uanze, hapana budi malalamiko yaliyoandikwa yakabidhiwe kwa Mjumbe wa Timu ya Utendaji ya Jumuiya ya UEM aliyechaguliwa na mlalamikaji.
Iwapo hakuna Mjumbe wa Timu ya Utendaji anayeaminiwa na mlalamikaji, Mjumbe wa Baraza Kuu la Jumuiya ya UEM anaweza kuteuliwa kufanya hivyo ipasavyo.

- **a.** Mjumbe aliyeteuliwa anapaswa kuwasiliana na mshitakiwa/washitakiwa ndani ya kipindi cha wiki nne. Mteuliwa anaweza akapata ushauri kutoka nje iwapo itahitajika kufanya hivyo.
- **b.** Mteuliwa anatakiwa kutunza siri wakati wote wa mchakato wa uchunguzi kwa kiwango cha uchunguzi kinachostahiki na hatua rekebishi zinazofaa.
- **c.** Iwapo tuhuma zitathibitishwa, mteuliwa analazimika kupeleka ripoti kwa Katibu Mkuu au wasaidizi wake kwa ukweli wa jambo lililotokea.
- **d.** Iwapo watu hawa waliotajwa pia wanahusika katika shauri linalohusika Msimamizi Mkuu wa Jumuiya ya UEM au mmoja kati ya Manaibu wake anapaswa kuarifiwa.
- **e.** Iwapo tuhuma zimethibitishwa, shauri linapaswa kutolewa taarifa kwa mamlaka zenye weledi (ndani na nje ya jumuiya)
- **f.** Kwa nyongeza, Timu ya Utendaji na Baraza Kuu wanapaswa kuarifiwa kwa maandishi. Mamlaka husika itafanya uamuzi kuhusu hatua inayostahili.

## Shughuli za kuendelea

Jumuiya ya UEM hutoa vipindi vya mafunzo/taarifa kuhusu uzuiaji wa ubaguzi na ubaguzi wa kimbari, uongezakaji wa mwamko na taratibu za utoaji wa taarifa.  Watumishi wa Jumuiya wanahimizwa kushiriki katika uboreshaji endelevu wa utamaduni wa kufanya kazi.

# Kanuni Dhidi ya Ufisadi na kwa ajili ya Uwazi

**Jumuiya ya UEM imekubali Kanuni za Maadili dhidi ya Ufisadi na kwa ajili ya Uwazi kwa lengo la kuwajibika kwa vitendo kwa mujibu wa sheria na utaratibu wa kuigwa wa kijamii na kimaadili.**

## Fafanuzi

Ufisadi huleta madhara kwa jamii, ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya UEM. Kwa makusudi ya Kanuni hizi, ufafanuzi wa ufisadi ni uchukuliaji wowote wa kujinufaisha binafsi au wa mtu wa tatu kwa kutumia vibaya sifa na mamlaka aliyopewa. Hii inajumuisha utoaji, uombaji au upokeaji wa zawadi, mikopo, tuzo au malipo kwa kazi maalumu. Pia inajumuisha utoaji au upokeaji wa manufaa yoyote kutoka kwa mtu wa tatu ili aweze kufanya jambo fulani kinyume cha uaminifu, kinyume cha sheria au kutoaminika tena.

### Malengo ya Kanuni za Maadili ni

- Kuzuia na kupambana na ufisadi kwa vitendo. Hii inatumika katika uhusiano wowote unaotumika katika uhusiano wa kimkataba na kiubia ambamo Jumuiya ya UEM imehusika.
- Kuzingatia kwa dhati dhana ya Hadhi na Uwazi ya taswira binafsi ya Jumuiya ya UEM na kulifanya jambo hili kuwa lenye kumhusu kila mdau wa Jumuiya ya UEM.

Ili kufikia malengo yake, Kanuni za Maadili hazina budi kuwa nguzo kuu ya ushirikiano wote.

## Maeneo ya kutumika:

Kanuni hizi za Maadili zinatumika katika mazingira na shughuli zote za Jamii ya UEM. Hii ni inahusisha waajiriwa, watu wanaowakilisha Jumuiya ya UEM na shughuli zingine zozote zinazofanyika kwa niaba ya Jumuiya ya UEM.

## Mapendekezo ya jinsi ya utumiaji;

### Wachunguzi wa Malalamiko

Baraza Kuu la Jumuiya ya UEM linateua Mchunguzi wa Malalamiko kwa kila mkoa. Hawa ni watu wasio na upendeleo ambao wanahusika kuhudumu kama wasuluhishi katika masuala mbalimbali.

### Wajibu:

Waajiriwa wote na wengineo wanaohusiana na Jumuiya ya UEM wana wajibu wa kukataa kuburuzwa katika vitendo vya tuhuma za ufisadi. Vilevile wanayo haki na wajibu wa kutoa taarifa kuhusu kitendo chochote cha ufisadi wanachokijua au wanachohisi dalili zake kwa Mchunguzi wa Malalamiko mhusika au kwa mjumbe wa Timu ya Uendeshaji. Iwapo Mchunguzi wa Malalamiko atajua tuhuma hizo au atahisi kuwepo kwa ufisadi, atalazimika kumwarifu Katibu Mkuu mara moja. Iwapo tuhuma zinamhusu Katibu Mkuu, Msimamizi Mkuu (Moderator) ataarifiwa. Wachunguzi wa Malalamiko wanapaswa pia kila mwaka kukabidhi taarifa kwenye Baraza Kuu.

Katibu Mkuu anapaswa kujadili na Timu ya Utendaji tuhuma zozote za ufisadi ambazo yeye anajua. Katibu Mkuu ataamua ndani ya mwezi mmoja jinsi tuhuma za ufisadi zitakavyochunguzwa. Katibu Mkuu anaweza kuteua Tume ya watu wa tatu kuchunguza tuhuma. Iwapo tuhuma zinamhusu Katibu Mkuu, Msimamizi Mkuu mwenyewe anawajibika kuchunguza tuhuma hizo.

Baada ya kukamilisha uchunguzi, ambao hautazidi mwaka mmoja, ripoti itakabidhiwa kwenye Baraza, ikizingatia kwa makini uhifadhi wa data na usiri wa ripoti hiyo. Ripoti hiyo itajadiliwa katika Kamati ya Fedha ya Baraza Kuu.

Iwapo tuhuma za ufisadi zitathibitishwa, mtu anayehusika atachukuliwa hatua za kisheria zinazowezekana dhidi ya mkosaji/wakosaji kwa mujibu wa sheria husika za nchi.

## Shughuli za kuendelea

Jumuiya ya UEM hutoa vipindi vya mafunzo/taarifa kuhusu uwazi na uzuiaji ufisadi, uongezakaji wa mwamko na taratibu za utoaji wa taarifa. Watumishi wa Jumuiya wanahimizwa kushiriki katika uboreshaji endelevu wa utamaduni wa kufanya kazi.

# Give a hint

If you have discovered violations of these CoCs and would like to report them, please do so via our website. We guarantee protection for whistleblowers and professional and careful processing:

**www.vemission.org/en/whistleblower-protection-act**

SW 11-2025

VEM
**UNITED EVANGELICAL MISSION**
Communion of Churches in three Continents


**Indonesia**
Jl. Pdt. J. Wismar Saragih
Bane, Kec. Siantar Utara
Kota Pematangsiantar (101)
North Sumatera 21142
+62-(0)-61-7332470
asiaregional@vemission.org

**Tanzania**
Luther House, Fifth floor
Sokoine Drive
PO Box 75240
Dar es Salaam
+255-222-125980
africaregional@vemission.org

**Germany**
Rudolfstraße 137
42285 Wuppertal
+49 202 890 04-0
info@vemission.org


**www.vemission.org**

#unitedinmission


Initiative Transparente Zivilgesellschaft

DZI Spenden-Siegel Zeichen für Vertrauen